**Issue no:** 01 | **Vol no:** 07 | **September** 2026: 102-110

# Mchango wa Vifo katika Ukuzaji wa Maudhui ya Riwaya ya *Chozi la Heri*

**Elizabeth Wayua Francis** (1)
**Rose Mavisi** (2)
**Lina Akaka** (3)

(1.2) Catholic University of Eastern Africa, Kenya; (3) Kirinyaga University, Kenya.
Main author's email: wayualiz01@gmail.com

**Article History**
Received: **2026.07.01**
Accepted: **2026.08.06**
Published: **2026.09.04**

**Cite this article in APA**
Francis, E. W., Mavisi, R., & Akaka, L. (2026). Mchango wa vifo katika ukuzaji wa maudhui ya riwaya ya *Chozi la Heri*. *Editon consortium journal of Kiswahili, 7*(1), 102–110. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.746

**Ikisiri**
Utafiti huu ulilenga kubainisha namna maudhui ya kifo yanavyochangia ukuzaji wa maudhui mengine katika riwaya *Chozi la Heri* ya Assumpta K. Matei. Katika fasihi, maudhui ya kifo hayajitokezi kama maudhui yanayojitegemea pekee, bali hutumika kama nyenzo ya kuibua, kuendeleza na kuimarisha maudhui mengine yanayohusu maisha na jamii. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Udhanaishi kwa mujibu wa Sartre (1948) na ulitumia muundo wa kimaelezo. Data za msingi zilikusanywa kutoka *Chozi la Heri*, iliyoteuliwa kimakusudi, huku data za sekondari zikikusanywa maktabani kutoka vitabu, majarida na tasnifu zinazohusiana na mada. Data zilichanganuliwa kimaelezo kwa kuongozwa na mhimili teule wa Nadharia ya Udhanaishi na kuwasilishwa chini ya mada ndogo zilizotokana na maudhui yaliyobainika. Matokeo yalionyesha kuwa maudhui ya kifo yalichangia ukuzaji wa maudhui ya ukoloni mkongwe, ukoloni mamboleo, uongozi mbaya, dini, dhuluma, ukatili na mitazamo ya jamii kuhusu jinsia ya kiume. Utafiti huu unatarajiwa kuwanufaisha wanafunzi, walimu, wahakiki na wanazuoni wa fasihi ya Kiswahili kwa kupanua uelewa kuhusu namna maudhui ya kifo yanavyohusiana na kukuza maudhui mengine katika kazi za fasihi.

**Maneno muhimu:** Kifo, maudhui, riwaya, udhanaishi.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Katika fasihi, maudhui hujengwa na kuendelezwa kupitia uhusiano wa karibu kati ya matukio, wahusika na migogoro mbalimbali (Gradin, 2021). Uhusiano huu huwezesha maudhui moja kuchochea, kuibua na kuimarisha maudhui mengine, hivyo kujenga maana pana ya kazi ya kifasihi. Miongoni mwa maudhui yanayoweza kuwa kichocheo cha maudhui mengine ni maudhui ya kifo, ambayo hujitokeza si kama mwisho wa maisha ya mhusika pekee, bali pia kama tukio linalosababisha mabadiliko ya matukio, migogoro na mitazamo ya wahusika. Kwa hiyo, kuchunguza maudhui ya kifo kunahitaji kuangalia pia maudhui mengine yanayoibuka au kuendelezwa kutokana na vifo vinavyosawiriwa katika kazi ya kifasihi. Brooks na Warren (1943) anaeleza kuwa kila tukio katika simulizi hupata umuhimu kutokana na mchango wake katika kujenga maana ya kazi nzima, ilhali Eagleton (1996) anaonyesha kuwa fasihi huakisi hali halisi ya maisha ya jamii kupitia maudhui yanayojengwa katika kazi za kifasihi. Kwa msingi huo, utafiti wa maudhui ya kifo katika fasihi unapaswa kuzingatia namna kifo kinavyohusiana na kuendeleza maudhui mengine badala ya kukichukulia kama dhamira inayojitegemea.

Katika fasihi ya Kiafrika, waandishi wametumia maudhui ya kifo kama msingi wa kuibua na kuendeleza masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Irele (2001) anaonyesha kuwa katika *Things Fall Apart* ya Chinua Achebe, kifo cha Okonkwo kinahusishwa na migogoro ya kitamaduni, ukoloni na mtanziko wa utambulisho wa Mwafrika. Vivyo hivyo, Soyinka (1975) anaeleza kuwa kifo katika fasihi ya Kiafrika ni sehemu ya mjadala mpana kuhusu maisha, haki, utamaduni na mabadiliko ya kijamii. Hoja hizi zinaonyesha kuwa kifo kinaweza kuwa chanzo cha kuibuka kwa maudhui mengine na hivyo kuchangia katika ujenzi wa ujumbe mpana wa kazi ya fasihi.

Katika fasihi ya Kiswahili, maudhui ya kifo pia yamehusishwa na ujenzi wa maudhui mengine. Mirieri (1993), katika uchunguzi wake wa kifo katika riwaya teule za Kiswahili, alibainisha kuwa kifo hutumika kuendeleza maudhui yanayohusiana na migogoro ya kijamii, dhuluma na ukandamizaji. Odongo (2014) naye alibaini kuwa kifo katika mashairi teule ni mhimili unaochochea na kukuza dhamira nyingine. Mose na Obuchi (2021) walionyesha kuwa kifo hutumiwa kama motifu ya kifasihi inayounganisha matukio, kuibua migogoro na kuendeleza dhamira za kijamii na kifalsafa. Tafiti hizi zinaonyesha uhusiano kati ya kifo na maudhui mengine, lakini zimejikita katika riwaya teule kwa ujumla au ushairi na katika kuangalia kifo kama motifu au kifaa cha utunzi. Hivyo, bado kuna haja ya kuchunguza kwa mtazamo mahususi namna maudhui ya kifo yanavyochangia moja kwa moja ukuzaji wa maudhui mbalimbali ndani ya riwaya mahususi ya Kiswahili.

Kwa msingi wa pengo hilo, makala hii inachunguza namna maudhui ya kifo yanavyochangia ukuzaji wa maudhui mengine katika *Chozi la Heri* (Matei, 2014). Uchunguzi unaangazia namna vifo vinavyosawiriwa katika riwaya vinavyokuwa kichocheo cha kuibua na kuendeleza maudhui ya ukoloni, uongozi mbaya, dini, dhuluma, ukatili na mitazamo ya jamii kuhusu jinsia ya kiume. Kwa kufanya hivyo, makala inaonyesha kuwa maudhui ya kifo hayajitokezi kama mwisho wa maisha ya wahusika pekee, bali yana nafasi muhimu katika kujenga maana, ujumbe na maudhui mengine ya riwaya.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Katika fasihi, kifo ni mojawapo ya maudhui yanayoweza kuchangia ujenzi na ukuzaji wa maudhui mengine kama vile haki, maadili, migogoro ya kijamii, dini na falsafa ya maisha. Tafiti mbalimbali zimechunguza nafasi ya kifo katika kazi za kifasihi kutoka mitazamo na miktadha tofauti. Hata hivyo, tafiti hizo zinatofautiana katika namna zinavyohusianisha kifo na maudhui mengine, aina ya kazi za kifasihi zilizochunguzwa na nadharia zilizotumika. Uchambuzi wa tafiti hizo unaonyesha kuwa, ingawa kifo kimejadiliwa kama chanzo cha kuibuka kwa maana na maudhui mbalimbali, bado kuna haja ya kueleza kwa kina uhusiano wa moja kwa moja kati ya matukio ya vifo na ukuzaji wa maudhui mengine katika riwaya mahususi ya Kiswahili.

Mirieri (1993) alichunguza nafasi ya kifo katika riwaya za *Kiu*, *Nyota ya Rehema*, *Kasri ya Mwinyi Fuad* na *Kuli*. Alibaini kuwa kifo hutumika kuibua migogoro ya kijamii, kufichua dhuluma na ukosefu wa haki, hivyo kuchangia katika kuendeleza maudhui ya kijamii. Utafiti huu una umuhimu kwa utafiti wa sasa kwa sababu unaonyesha mapema uhusiano kati ya kifo na maudhui mengine katika riwaya ya Kiswahili. Hata hivyo, Mirieri alijikita katika riwaya kadhaa na kuangalia zaidi nafasi ya kifo katika ujenzi wa maudhui kwa mtazamo wa uyakinifu wa kijamii. Utafiti wa sasa unaendeleza maarifa hayo kwa kuchunguza kwa namna mahususi jinsi matukio ya vifo yanavyokuwa kichocheo cha kuibua maudhui mbalimbali katika *Chozi la Heri* (Matei, 2014), kwa kuongozwa na Nadharia ya Udhanaishi. Hivyo, licha

ya Mirieri kuweka msingi wa kuhusianisha kifo na maudhui ya kijamii, bado haijaelezwa kwa kina namna vifo vinavyohusishwa na maudhui mahususi yanayojitokeza katika riwaya ya Matei (2014).

Freytag na Ramasubramanian (2019) walichunguza namna kifo kinavyowasilishwa katika tamthilia za kitabibu za televisheni kwa kuzingatia wahusika wanaokufa, sababu za vifo, muundo wa simulizi na dhamira zinazojitokeza. Walibaini kuwa kifo ni nyenzo muhimu ya kuendeleza maudhui kama maadili, uwajibikaji wa kitabibu, uhusiano wa kijamii na ukuaji wa wahusika. Matokeo yao yanaimarisha hoja kwamba kifo hakiishii katika kuonyesha mwisho wa maisha, bali kinaweza kuwa kichocheo cha kuendeleza maana na maudhui mengine katika simulizi. Tofauti na utafiti wa sasa, wao walijikita katika tamthilia za televisheni na kutumia nadharia ya usimulizi, ilhali utafiti huu unachunguza riwaya ya Kiswahili kwa kutumia Nadharia ya Udhanaishi. Zaidi ya hayo, utafiti wao ulijikita katika muktadha wa kitabibu, hivyo haukuonyesha namna vifo vinavyoweza kuchochea maudhui mapana ya kijamii na kisiasa kama ukoloni, uongozi mbaya, ufisadi, dhuluma, ukatili na mitazamo ya jamii kuhusu jinsia ya kiume. Kwa hiyo, utafiti wa sasa unapanua maarifa hayo kwa kuonyesha namna kifo kinavyoweza kuwa chanzo cha kuibuka kwa maudhui mbalimbali katika riwaya ya Kiswahili.

Mose na Obuchi (2021) walichunguza kikale cha kifo kama mbinu ya utunzi katika fasihi ya Kiswahili. Walibaini kuwa kifo ni motifu muhimu inayounganisha matukio ya simulizi, kuibua migogoro na kuendeleza dhamira za kijamii na kifalsafa. Utafiti wao unaafikiana na utafiti wa Mirieri (1993) kwa kusisitiza kuwa kifo hakijitokezi kama tukio la mwisho wa maisha pekee, bali kinaweza kuwa chombo cha kuendeleza maana pana ya kazi ya fasihi. Hata hivyo, Mose na Obuchi walikichunguza kifo zaidi kama kikale na mbinu ya utunzi kwa kutumia nadharia ya uhakiki wa vikale. Utafiti wa sasa unatofautiana nao kwa kulenga uhusiano wa kifo na maudhui mengine katika *Chozi la Heri* (Matei, 2014), badala ya kukichunguza zaidi kama motifu ya kifasihi. Pengo linalojitokeza hapa ni kwamba, ingawa Mose na Obuchi wanaonyesha kuwa kifo huibua migogoro na dhamira, hawajaeleza kwa kina namna kila tukio la kifo linavyoweza kuchochea maudhui mahususi ya kijamii yanayojitokeza baadaye katika simulizi. Utafiti huu unalenga kujaza pengo hilo.

Nicholas (2023) alichunguza dhamira ya kifo katika *Utenzi wa Inkishafi* kwa mtazamo wa kidini na kimaadili. Alibaini kuwa kifo hutumiwa kuonyesha ubatili wa maisha ya dunia, kuonya na kufundisha maadili, pamoja na kumkumbusha mwanadamu kuhusu mwisho wa maisha. Utafiti huu unaonyesha kuwa kifo kinaweza kuwa chanzo cha tafakuri na maudhui mengine badala ya kuwa tukio la mwisho wa maisha. Hata hivyo, Nicholas alijikita katika ushairi wa kale na hasa katika mitazamo ya kidini na kimaadili kuhusu kifo. Kwa upande mwingine, utafiti wa sasa unachunguza riwaya ya Kiswahili na kuangalia kwa upana zaidi namna vifo vinavyochangia ukuzaji wa maudhui ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kijinsia. Kwa hiyo, utafiti wa Nicholas unaweka msingi wa kuelewa uhusiano kati ya kifo na maudhui ya maadili na falsafa, lakini haujibu kikamilifu swali la namna matukio ya vifo yanavyoweza kuchochea maudhui mbalimbali ndani ya riwaya ya Kiswahili.

Korhonen (2023) alichunguza uwasilishaji wa kifo na huzuni katika riwaya *In a Monster Calls* na *The Honest Truth* ili kubaini namna dhamira ya kifo inavyojenga simulizi na kuathiri msomaji. Alibaini kuwa kifo hujenga huruma, uelewa wa kijamii na tafakuri kuhusu maisha, hasa kinapohusishwa na upendo, msamaha na matumaini. Matokeo haya yanaonyesha kuwa kifo kina athari zinazovuka tukio la kufariki kwa mhusika na kinaweza kuibua mitazamo na hisia zinazohusiana na maudhui mengine. Hata hivyo, utafiti wa Korhonen ulijikita katika fasihi ya watoto na vijana na ulilenga zaidi athari za kifo katika ujenzi wa simulizi na uzoefu wa msomaji. Tofauti na utafiti huo, utafiti huu unachunguza namna vifo vinavyotumiwa na mwandishi kama kichocheo cha kuibua na kuendeleza maudhui mengine ya kijamii katika riwaya ya Kiswahili. Hivyo, maarifa yanayokosekana katika utafiti wa Korhonen ni uchanganuzi wa kina wa mchakato ambao tukio la kifo husababisha au kuchochea kuibuka kwa maudhui mahususi ndani ya kazi ya kifasihi.

Kwa jumla, tafiti za Mirieri (1993), Freytag na Ramasubramanian (2019), Mose na Obuchi (2021), Nicholas (2023) na Korhonen (2023) zinaonyesha kwa pamoja kuwa kifo kinaweza kuwa kichocheo cha kuibua na kuendeleza maana, migogoro na maudhui mengine katika kazi za kifasihi. Mirieri (1993) na Mose na Obuchi (2021) wanaweka msingi muhimu katika fasihi ya Kiswahili kwa kuonyesha uhusiano wa kifo na ujenzi wa maudhui, huku Freytag na Ramasubramanian (2019) wakionyesha namna kifo kinavyoweza kuendeleza maudhui ya maadili na mahusiano ya kijamii. Nicholas

(2023) anaonyesha mchango wa kifo katika maudhui ya kimaadili na kifalsafa, ilhali Korhonen (2023) anaonyesha uwezo wa kifo wa kuibua huruma na tafakuri kuhusu maisha. Hata hivyo, tafiti hizi hazijaeleza kwa kina namna matukio mahususi ya vifo yanavyosababisha kuibuka na kuendelezwa kwa maudhui mbalimbali ya kijamii katika riwaya Matei (2014). Aidha, tafiti zilizotajwa zimejikita katika miktadha, tanzu na mitazamo tofauti, hivyo kuacha pengo la kimaarifa kuhusu uhusiano wa moja kwa moja kati ya maudhui ya kifo na ukuzaji wa maudhui mengine katika riwaya hiyo. Kutokana na pengo hilo, utafiti huu ulilenga kuchunguza namna maudhui ya kifo yanavyochangia ukuzaji wa maudhui ya ukoloni mkongwe, ukoloni mamboleo, uongozi mbaya, dini, dhuluma, ukatili na mitazamo ya jamii kuhusu jinsia ya kiume katika *Chozi la Heri*.

**Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Udhanaishi kwa mujibu wa Sartre (1948). Kwa mujibu wa Sartre, binadamu huzaliwa bila hatima au maana ya awali, hivyo hujijengea maana ya maisha kupitia uhuru wa kufanya maamuzi na kuwajibikia matokeo ya maamuzi yake. Aidha, Sartre anakiona kifo kuwa hali isiyoepukika katika uwepo wa binadamu inayomfanya kutafakari kuhusu maisha, uhuru, wajibu na hali yake ya kuwepo duniani. Kwa mtazamo huu, maisha ya binadamu yanaweza kuhusisha mateso, changamoto, hofu na kukata tamaa, ambazo humlazimisha binadamu kutafakari hali yake na maana ya maisha. Kuhusiana na hoja hiyo, Kierkegaard (1997) alisisitiza nafasi ya imani katika kumwezesha binadamu kupata maana ya maisha na kukabiliana na changamoto za uwepo wake. de Beauvoir (1949; 1997) aliendeleza mawazo ya udhanaishi kwa kueleza kuwa uhuru wa binadamu hujengwa kupitia maamuzi yake, ingawa maamuzi hayo huathiriwa na mazingira ya kijamii na kihistoria. Naye Judaken na Bernasconi (2012) wanaeleza kuwa, kwa mtazamo wa Sartre, binadamu hana hatima iliyopangwa bali hujenga maana ya maisha kupitia uchaguzi wake hata anapokabiliwa na mateso, changamoto na kifo.

Nadharia hii inajengwa katika mihimili inayohusiana na uhuru wa binadamu wa kujijengea maana ya maisha kupitia maamuzi yake, kifo kama hatima isiyoepukika ya kila binadamu, imani kama mojawapo ya njia za kutafuta maana ya maisha, na kukata tamaa kunakotokana na kutambua mipaka ya uwezo wa binadamu. Mihimili hii ina umuhimu katika utafiti huu kwa sababu inamwezesha mtafiti kulitazama tukio la kifo zaidi ya mwisho wa uhai wa mhusika. Kwa mtazamo huu, kifo kinaweza kuchukuliwa kama tukio linalomweka binadamu katika hali ya kutafakari kuhusu maisha, uhuru, wajibu na maana ya kuwepo kwake. Hivyo, mhimili huu uliuwezesha utafiti kuchanganua uhusiano kati ya tukio la kifo, mateso yanayowapata wahusika na maudhui mengine yanayojengwa kutokana na matukio hayo. Kwa msingi huo, Nadharia ya Udhanaishi ilitumika kama msingi wa kueleza kwamba vifo katika *Chozi la Heri* si matukio ya mwisho wa maisha pekee, bali ni vichocheo vinavyomweka binadamu katika hali ya mateso na tafakuri, ambayo mwandishi huitumia kukuza maudhui mengine ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kifalsafa.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo kwa kuwa uliwezesha kueleza na kutafsiri kwa kina namna vifo vinavyojitokeza katika matini ya kifasihi na jinsi vinavyochangia ukuzaji wa maudhui mengine. Muundo huu ulifaa kwa utafiti kwa sababu data zilizochanganuliwa zilikuwa za kimaandishi na zilihitaji kuelezwa na kufasiriwa kulingana na muktadha wa matukio, wahusika na maudhui yanayojitokeza katika riwaya. Eneo la utafiti lilihusu fasihi ya Kiswahili, hususan tanzu ya riwaya, huku kundi lengwa likiwa ni riwaya za Kiswahili zinazohusisha maudhui ya kifo. Sampuli ya utafiti ilikuwa riwaya *Chozi la Heri* (Matei, 2014), iliyoteuliwa kwa kutumia usampulishaji wa kimakusudi kwa sababu inajumuisha matukio mbalimbali ya vifo yanayohusishwa na maudhui mengine ya kijamii, hivyo kutoa data inayotosheleza kujibu lengo la utafiti. Chanzo cha data za msingi kilikuwa matini ya Matei (2014), ambayo ilisomwa kwa makini zaidi ya mara moja na kunakiliwa sehemu zinazohusiana na lengo la utafiti. Data za sekondari zilikusanywa kupitia mapitio ya maandiko kutoka vitabu, majarida na tasnifu zinazohusiana na mada. Vyanzo hivi vilitumika hasa kujenga msingi wa kinadharia na kitaaluma wa utafiti, kulinganisha matokeo na tafiti zilizotangulia, na kusaidia katika kutafsiri na kujadili data iliyopatikana. Data zilizokusanywa zilipangwa kulingana na mada ndogo zilizobainika, kisha zikafasiriwa na kuchanganuliwa kimaelezo kwa kuongozwa na mhimili teule wa Nadharia ya Udhanaishi na maoni ya wataalamu mbalimbali.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Sehemu hii inawasilisha na kujadili matokeo ya utafiti kuhusu namna maudhui ya kifo yanavyochangia ukuzaji wa maudhui mengine katika riwaya ya *Chozi la Heri (Matei, 2014)*. Uchanganuzi unaonyesha kuwa kifo hakijitokezi tu kama tukio la mwisho wa maisha, bali kama nyenzo muhimu ya kifani inayochochea kuibuka na

kuendelezwa kwa dhamira na maudhui mengine. Kwa hivyo, uchanganuzi unaofuata unaonyesha jinsi visa vya vifo vilivyotumiwa na mwandishi kama nyenzo ya kuibua na kukuza maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika riwaya ya Matei (2014).

**Ukoloni Mkongwe**

Maudhui ya ukoloni mkongwe yanajitokeza baada ya kifo cha familia ya Ridhaa, ambacho kinamrudisha katika kumbukumbu za mazungumzo yake na Tila kuhusu historia ya kunyang'anywa ardhi za Waafrika. Hivyo, msiba wa Ridhaa ndio unaochochea kuibuka kwa maudhui haya, kwani kupitia majonzi yake mwandishi anafichua historia ya dhuluma za kikoloni. Ridhaa anakumbuka akisema:

> *Sheria ya mkoloni ilipompa Mzungu kibali cha kumiliki mashamba... Waafrika walilazimika kuwa vibarua katika mashamba yaliyokuwa yao au maskwota...* (Matei, 2014, uk. 7)

Dondoo hili linaonyesha namna ukoloni mkongwe ulivyowanyang'anya Waafrika ardhi yao na kuwafanya kuwa vibarua katika mashamba yaliyokuwa mali yao. Matumizi ya maneno kama *"maskwota"* na *"vibarua"* yanaonyesha ukandamizaji, unyonyaji na ukosefu wa usawa uliotokana na sera za kikoloni. Kifo cha familia ya Ridhaa kinakuwa daraja la kurejelea historia hii, hivyo kuifanya dhamira ya ukoloni ijitokeze kwa nguvu zaidi. Hoja hii inaafikiana na mawazo ya Mose na Obuchi (2021) kwamba kifo ni motifu inayounganisha matukio na kuendeleza dhamira kuu za kijamii.

Kwa mujibu wa Beauvoir (2010), uhuru wa kweli unahusisha kuheshimu utu na haki za wengine. Hata hivyo, mfumo wa kikoloni uliwanyima Waafrika haki hiyo kwa kuwanyang'anya ardhi na kuwafanya watumwa wa kiuchumi katika nchi yao wenyewe. Ridhaa anapotafakari historia hii baada ya kufiwa na familia yake, mwandishi anaonyesha kuwa madhara ya ukoloni bado yanaendelea kuathiri maisha ya wananchi hata baada ya uhuru. Kwa hiyo, kifo kinatumika kama kichocheo cha kuibua maudhui ya ukoloni mkongwe na kufichua historia ya ukandamizaji wa Waafrika.

**Athari za Ukoloni Mamboleo**

Maudhui ya ukoloni mamboleo yanadhihirika kupitia tafakuri ya Ridhaa kuhusu hali ya kiuchumi ya taifa baada ya kupoteza familia yake. Kifo cha familia yake kinabadilisha mtazamo wa Ridhaa kutoka kwenye majonzi ya msiba binafsi hadi kutafakari mateso na changamoto zinazoikumba jamii yake kwa ujumla. Katika hali hiyo ya majonzi, Ridhaa anakumbuka mazungumzo yake na marehemu bintiye Tila kuhusu umiliki wa ardhi na uchumi wa taifa. Mwandishi anasema:

> *Je, miaka hamsini ya uhuru imetukuza kiuchumi?... Hatuna tunalomiliki. Wageni ndio wanaoamua wakuze nini katika ardhi yetu!* (Matei, 2014, uk. 6)

Kauli hii inadhihirisha kuwa uhuru wa kisiasa haujaondoa utegemezi wa kiuchumi, kwani wageni bado wana ushawishi mkubwa katika umiliki na matumizi ya rasilimali za taifa. Hivyo, kifo cha familia ya Ridhaa kinachangia ukuzaji wa maudhui ya ukoloni mamboleo kwa kumweka mhusika katika hali ya tafakuri inayompelekea kuona uhusiano kati ya msiba wake binafsi na matatizo mapana ya jamii. Kifo hakisababishi ukoloni mamboleo moja kwa moja, bali kinakuwa kichocheo cha kumbukumbu na tafakuri inayoufichua mfumo huo wa utegemezi wa kiuchumi.

Mtazamo huu unaafikiana na Sartre (1948), anayeeleza kuwa mwanadamu hukabiliwa na mateso na changamoto zisizoepukika zinazomlazimisha kutafakari kuhusu maisha na hali yake ya kuwepo. Ridhaa, akiwa amepoteza familia yake, anakabiliwa na mateso yanayomfanya asiishie kuomboleza waliokufa, bali ajiulize kuhusu mazingira ya kijamii na kiuchumi yanayowazunguka. Kwa hiyo, kifo cha familia yake kinapanua upeo wa mateso kutoka kwenye hasara ya mtu binafsi hadi kwenye tafakuri ya mateso ya jamii nzima, ambapo wananchi wanaendelea kuwa wategemezi licha ya taifa kuwa limepata uhuru wa kisiasa.

Aidha, kumbukumbu hii inaonyesha kuwa ukoloni mamboleo katika *Chozi la Heri* hauwasilishwi kwa maelezo ya moja kwa moja pekee, bali unafichuliwa kupitia athari za kifo kwa fikra za mhusika. Ridhaa anapokumbuka kuwa "hatuna tunalomiliki" na kwamba "wageni ndio wanaoamua" kuhusu uzalishaji katika ardhi yao, msomaji anatambua kuwa tatizo linalomkabili Ridhaa linaenda zaidi ya msiba wa familia yake. Kifo kinakuwa njia ya kumwongoza mhusika na msomaji kutoka kwenye tukio la kibinafsi la kupoteza familia hadi kwenye suala pana la utegemezi, unyonyaji na ukosefu wa uhuru wa kiuchumi. Kwa hivyo, katika sehemu hii, mchango wa kifo katika ukuzaji wa ukoloni mamboleo unaonekana zaidi katika kuibua tafakuri na kufichua uhusiano kati ya mateso binafsi ya Ridhaa na mfumo mpana wa utegemezi wa kiuchumi katika jamii ya baada ya uhuru.

**Uongozi Mbaya**

Maudhui ya uongozi mbaya yanajitokeza kama mojawapo ya dhamira kuu zinazojengwa kupitia vifo katika *Chozi la Heri* (Matei, 2014). Hili ni jambo la kawaida katika fasihi kama wanavyodai Freytag Ramasubramanian (2018) kwamba kifo katika fasihi hutumiwa kufichua migogoro ya kijamii, ukandamizaji na kushindwa kwa mifumo ya uongozi.

Mwandishi anaonyesha kuwa vifo vingi vinavyowapata wahusika havitokani na majanga ya kawaida pekee bali pia na kushindwa kwa viongozi kutekeleza wajibu wao kwa uwajibikaji, haki na uadilifu. Kupitia matukio ya vurugu, ukandamizaji na matumizi mabaya ya mamlaka, kifo kinatumika kufichua athari za uongozi usiojali maisha ya wananchi.

Maudhui haya yanaonekana kupitia vifo vya mamia ya watu kutokana na vurugu zinazozuka baada ya uchaguzi kati ya wafuasi wa Mwekevu na wa mpinzani wake. Vurugu hizo zilisababisha vifo vya mamia ya wafuasi hao huku viongozi hao wakijitenga na kukosa kuingilia kati. Mwandishi anaeleza:

> *Vilio vya Kite vilihanikiza hewani, vita vikaanza kati ya kundi lililounga mkono uongozi wa Mwekevu na lile lililomuunga mkono mpinzani wake mwanamume...* (Matei, 2014, uk. 18)

Baadaye anasema:
"Mamia ya roho zisizo na hatia zilisalimu amri chini ya pambaja za risasi na mapigo ya rungu..." (Matei, 2014, uk. 19)

Maneno hayo yanaonyesha kuwa tamaa ya madaraka na kushindwa kwa viongozi kudumisha amani husababisha umwagikaji wa damu na mateso ya wananchi wasiokuwa na hatia. Wakati viongozi wakijificha majumbani mwao, wananchi ndio wanaouawa na kujeruhiwa. Kwa mujibu wa Beauvoir (1996)**,** mamlaka yanapotumika kukandamiza uhuru wa wengine huzalisha dhuluma na ukosefu wa haki.

**Dini**

Maudhui ya dini yanajitokeza kwa kina katika riwaya ya *Chozi la Heri (Matei, 2014)* kupitia matukio ya kifo, mateso na maafa yanayowakumba wahusika. Mwandishi anaonyesha kuwa kifo humsukuma mwanadamu kumtegemea Mungu, kutafuta faraja ya kiroho na kujenga matumaini mapya baada ya maumivu. Hivyo, dini inajengwa kama chanzo cha uvumilivu, uponyaji wa nafsi na imani kwamba hata baada ya kifo na mateso, maisha yanaweza kuendelea. Mtazamo huu unaafikiana na Kierkegaard (1997) anayesema kuwa mwanadamu hupata utulivu wa nafsi kwa kumtegemea Mungu anapokabiliwa na mateso na hofu ya kifo.

Maudhui haya yanajitokeza kupitia vifo vya wanafamilia wa mhusika Ridhaa, walioangamia kutokana na mkasa wa moto pamoja na mali zake. Mwandishi anasema:

> *Aliweza kuudhibiti ugonjwa wa shinikizo la damu ambao ulitokana na mshtuko wa kupoteza jamaa na mali yake dafrao moja. Awali akijihisi kama yule Ayub kwenye kitabu kitakatifu ambaye ibilisi aliifakamia familia na mali yake takriban kutwa moja.* (Matei, 2014, uk. 36)

Kupitia maneno hayo, Ridhaa anajilinganisha na Ayubu wa Biblia, ishara kwamba anatafuta faraja kupitia imani ya kidini baada ya kukumbwa na maafa. Kifo kinakuwa kichocheo cha tafakuri kuhusu uwezo wa Mungu na udhaifu wa mwanadamu mbele ya mauti. Badala ya kukata tamaa, Ridhaa anapata nguvu ya kuendelea kuishi kupitia mfano wa Ayubu aliyestahimili majaribu kwa imani. Hali hii inaafikiana na Korhonen (2023) anayeeleza kuwa kifo katika fasihi huibua tafakuri kuhusu maana ya maisha na mateso, huku Nicholas (2023) akionyesha kuwa humkumbusha mwanadamu kuwa maisha ni ya muda mfupi.

**Dhuluma na Ukatili**

Maudhui ya dhuluma na ukatili yanajitokeza wazi katika *Chozi la Heri*, ambapo kifo kinatumika kama nyenzo ya kukuza dhamira hizi kwa kufichua mateso, ukandamizaji na ukosefu wa haki katika jamii. Wahusika wengi hukumbwa na unyanyasaji wa kimwili, kihisia na kijamii unaosababishwa na chuki, husuda, matumizi mabaya ya mamlaka na ukosefu wa huruma. Kwa mujibu wa Sartre (1948), maisha ya binadamu hujaa mateso na changamoto zinazomlazimisha kutafuta maana ya uwepo wake, hali inayodhihirika katika maisha ya wahusika wa riwaya hii. Dhuluma na ukatili vinaonekana kupitia mauaji ya familia ya Ridhaa yaliyofanywa na Mzee Kedi. Mwandishi anaeleza:
"Uuuui! Uuuui! Jamani tusaidieni!... Mzee Kedi, usituue, sisi tu majirani!" (Matei, 2014, uk. 3)

Kifo cha Terry, watoto wao na mjukuu Becky kinaonyesha kiwango cha unyama unaotokana na husuda na chuki. Ridhaa hubaki na majeraha makubwa ya kihisia akisema, "Familia yangu na mali yote hii kuteketea siku moja?" Tukio hili linaonyesha kuwa kifo kinatumika kufichua ukatili wa binadamu na athari zake kwa

walionusurika. Hoja hii inaafikiana na Mirieri (1993) kuwa kifo katika fasihi hufichua dhuluma na migogoro ya kijamii.

Dhuluma pia inaonekana baada ya kifo cha nyanya wa Chandachema. Baada ya kuishi kwa jirani, Satua anaanza kumtesa na kumfanya ajione mzigo:
"Ule uchangamfu aliokuwa nao Satua... uliyeyuka ghafla kama umande kwenye jua la asubuhi." (Matei, 2014, uk. 103)

Kifo cha nyanya kinakuwa chanzo cha ukatili wa kihisia na kijamii, kwani Chandachema hupoteza makazi, ulinzi na mapenzi ya kifamilia hadi kulazimika *"kujikabidhi kwa ulimwengu."* Mose na Obuchi (2021) wanaeleza kuwa kifo huchochea migogoro na kuendeleza dhamira mbalimbali za kifasihi, jambo linalodhihirika katika mateso ya Chandachema.

**Mitazamo ya Jamii Kuhusu Jinsia ya Kiume**

Katika riwaya ya *Chozi la Heri* (2014), jamii imemwekea mwanaume wajibu wa kuonekana mwenye nguvu, asiyeonyesha hisia na mwenye mamlaka. Mwandishi anaonyesha kuwa mfumo huu hauwaathiri wanaume, ambao hulazimika kuishi kulingana na matarajio ya jamii hata yanapowaletea mateso. Aidha, kifo kinatumika kama nyenzo muhimu ya kufichua madhara ya mfumo huu kwa kuonyesha jinsi maombolezo na huzuni vinavyodhibitiwa na mitazamo ya kijamii. Kwa mujibu wa Sartre (1948), binadamu ana uhuru wa kufanya maamuzi na kujijengea maana ya maisha, lakini uhuru huo huzuiwa na mitazamo ya kijamii inayomwekea masharti ya namna ya kuishi.

Mtazamo wa jamii kuhusu wanaume unajitokeza kupitia kifo cha familia ya mhusika Ridhaa baada ya kuteketea kwa moto. Badala ya kupewa nafasi ya kuomboleza kwa uhuru, Ridhaa anakumbushwa mafundisho ya mama yake kwamba mwanaume hafai kulia. Lakini baadaye, Ridhaa anashindwa kuyazuia machozi baada ya kuona majivu ya mkewe, wanawe, mkaza mwanawe na mjukuu wake Becky:

> *Ridhaa mwanangu, mwanaume hufumbika hisia. Machozi ya mwanamume hayapaswi kuonekana hata mbele ya majabali ya maisha... Leo hii Ridhaa hakujali la mama wala la baba... Sasa Ridhaa anatazamana na majivu ambayo bila shaka ni miili ya wanawe wawili, mkewe, mkaza mwanawe na mjukuu wake Becky.* (Matei, 2014, uk. 3 & 5)

Kupitia dondoo hili, mwandishi anadhihirisha kuwa mitazamo ya jamii humlazimisha mwanaume kuficha hisia zake hata katika majonzi makubwa. Kifo cha familia yake kinavunja matarajio hayo ya kijamii na kumfanya Ridhaa akubali ubinadamu wake kwa kulia. Hivyo, kifo kinatumika kufichua kuwa machozi si alama ya udhaifu bali ni sehemu ya kawaida ya maisha ya mwanadamu. Kwa mtazamo wa Sartre (1948), Ridhaa anatumia uhuru wake wa kujieleza licha ya mashinikizo ya mfumo potovu ya jamii.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho**: Kwa ujumla, utafiti huu ulibaini kuwa maudhui ya kifo katika *Chozi la Heri* hayajitokezi kama mwisho wa maisha ya wahusika pekee, bali hutumika kama nyenzo muhimu ya kisanaa inayochangia ukuzaji wa maudhui mengine. Kupitia visa vya vifo, mwandishi ameibua na kuendeleza maudhui ya ukoloni, uongozi mbaya, dini, dhuluma, ukatili na mitazamo ya kijamii kuhusu jinsia ya kiume, hivyo kuthibitisha kuwa kifo ni mhimili muhimu katika ujenzi wa maana na ujumbe wa riwaya. Kwa kuhitimisha, matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa visa vya vifo vimefungamanishwa kwa ustadi na hali halisi ya jamii, ambapo vinatumika kufichua changamoto za kijamii, kisiasa na kiuchumi zinazowakumba wahusika na jamii kwa ujumla. Hivyo, mjadala wa data ulithibitisha kuwa kifo si tukio la kusikitisha pekee, bali ni nyenzo muhimu ya kisanaa inayomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe na kuibua tafakuri kuhusu maisha na jamii.

**Mapendekezo:** Kutokana na matokeo hayo, inapendekezwa kuwa tafiti zaidi zifanywe kuhusu maudhui ya kifo katika tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili na kazi tofauti za kifasihi. Aidha, watafiti wachunguze mchango wa vipengele vingine vya fani na kutumia nadharia mbalimbali za uhakiki ili kupanua uelewa wa maudhui ya kifo. Vilevile, walimu wahimize uchambuzi wa uhusiano kati ya fani na maudhui katika ufundishaji wa fasihi, huku waandishi wakiendelea kutumia mbinu bunifu za kifani kushughulikia maudhui nyeti kama kifo ili kuelimisha jamii na kuchochea tafakuri kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii.

**REFERENCES**

Brooks, C., & Warren, R. P. (1943). *Understanding fiction*. Appleton-Century-Crofts.

de Beauvoir, S. (1949). *The ethics of ambiguity*. Philosophical Library. https://www.marxists.org/reference/subject/ethics/de-beauvoir/ambiguity/index.htm

de Beauvoir, S. (1996). *The ethics of ambiguity* (B. Frechtman, Trans.). Citadel Press.

de Beauvoir, S. (1997). *The second sex* (H. M. Parshley, Trans.). Vintage. https://atticbooks.co.ke/books/the-second-sex75

de Beauvoir, S. (2010). *The second sex* (C. Borde & S. Malovany-Chevallier, Trans.). Alfred A. Knopf.

Eagleton, T. (1996). *Literary theory: An introduction* (2nd ed.). Blackwell Publishers.

Freytag, J., & Ramasubramanian, S. (2019). Are television deaths good deaths? A narrative analysis of hospital death and dying in popular medical dramas. *Health Communication, 34*(7), 747–754. https://doi.org/10.1080/10410236.2018.1434735

Gradin, L. (2021, June 7). *7 types of conflict in literature: A writer's guide*. Reedsy. https://reedsy.com/blog/guide/conflict/

Irele, F. A. (2001). *The African imagination: Literature in Africa and the Black diaspora*. Oxford University Press. https://doi.org/10.1093/oso/9780195086188.001.0001

Judaken, J., & Bernasconi, R. (Eds.). (2012). *Situating existentialism: Key texts in context*. Columbia University Press. https://doi.org/10.7312/juda14774

Kierkegaard, S. (1997). *Christian discourses: The crisis and a crisis in the life of an actress* (H. V. Hong & E. H. Hong, Eds. & Trans.). Princeton University Press. https://doi.org/10.1515/9781400832385

Korhonen, M. (2023). *Representing death and grief in A Monster Calls and The Honest Truth* [Master's thesis, University of Eastern Finland]. University of Eastern Finland Repository. https://erepo.uef.fi/server/api/core/bitstreams/39a72a64-4980-4039-b4c3-169a5be5daf6/content

Matei, A. K. (2014). *Chozi la heri*. One Planet Publishing & Media Services Limited.

Mose, E. N., & Obuchi, S. M. (2021). Kikale cha kifo kama mbinu ya utunzi katika fasihi ya Kiswahili. *Mwanga wa Lugha, 6*(2), 151–158. https://journals.mu.ac.ke/index.php/mwl/article/view/251/210

Mirieri, E. R. O. (1993). *Kifo katika uendelezaji wa maudhui katika riwaya ya Kiswahili: Uchambuzi wa riwaya za Mohamed Suleiman Mohamed na Shafi Adam Shafi* [Thesis, University of Nairobi]. University of Nairobi Repository.

Nicholas, R. (2023). *Uhakiki wa utenzi wa Al-Inkishafi: Mtindo na maudhui yake*. Studocu. https://www.studocu.com/row/document/pwani-university/fasihi-ya-kiswahili/uhakiki-wa-utenzi-wa-al-inkishafi/51421797

Odongo, O. F. (2014). *Uchanganuzi wa uwasilishaji wa kifo katika mashairi teule ya Kiswahili* [Master's thesis, Maseno University]. Maseno University Repository.

Sartre, J.-P. (1948). *Existentialism and humanism* (P. Mairet, Trans.). Methuen.

Soyinka, W. (2002). *Death and the king's horseman*. W. W. Norton & Company.